# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

## TUME YA UTUMISHI WA UMMA

**MADA: MAJUKUMU YA TUME KATIKA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

***Imeandaliwa na:***
**Ofisi ya Rais,**
**Tume ya Utumishi wa Umma,**
**<u>DAR ES SALAAM</u>.**

**02 JUNI, 2017**

**MAJUKUMU YA TUME KATIKA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

## 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Utumishi wa Umma imeundwa chini ya Kifungu cha 9 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya Mwaka 2002 ambapo majukumu yake makubwa ni kusimamia na kuhakikisha kwamba Watumishi wa Umma, Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu zinazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika kusimamia masuala yanayohusu Rasilimali Watu pamoja na kushughulikia kwa wakati rufaa na malalamiko yanayowasilishwa Tume.

Majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ni kama ifuatavyo:-

(i) Kumshauri Rais kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yake aliyopewa kikatiba chini ya Ibara ya 36 kuhusu ujazaji wa nafasi zilizo wazi katika Utumishi wa Umma kadri Rais atakayohitaji

(ii) Kumshauri Rais kuhusu masuala ya Utumishi kadri atakavyohitaji

(iii) Kutoa miongozo na kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma

(iv) Kupokea na kushughulikia rufaa za mashauri yaliyotolewa maamuzi na Mamlaka za Nidhamu

(v) Kuwezesha, kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa watumishi wa Umma wa ngazi mbalimbali ili uwe wa ufanisi na wenye kuzingatia matokeo (result oriented)

(vi) Kuhakikisha kuwa Taratibu za Uendeshaji za Utumishi wa makundi mbalimbali zinatayarishwa na kutumika ipasavyo

(vii) Kuandaa na kuwasilisha kwa Rais taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Tume inayoonyesha shughuli zilizofanywa mwaka uliopita.

### 1.1 Mamlaka ya Tume

Mamlaka ya Tume ni kama ifuatavyo;-

(i) Kuwaita Watendaji Wakuu kutoa maelezo kuhusu utendaji kazi usioridhisha pale Tume inapokuwa na ushahidi au malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

(ii) Kuchukua hatua dhidi ya Watendaji Wakuu watakaoshindwa kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria watumishi wenye utendaji usioridhisha walio chini yao kwa kupitia Mamlaka zao za nidhamu.

(iii) Kuzitaka Mamlaka za Ajira kuwasilisha taarifa ambazo Tume itazihitaji kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME.

### 2.1 Kufanya Ukaguzi wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma

Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu zina wajibu mkubwa wa kusimamia masuala ya kiutumishi kwa Watumishi walio chini yao kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma.

Ili kuhakikisha kuwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu zinasimamia na kutekeleza masuala ya Rasilimali watu

ipasavyo, Tume hufanya Ukaguzi wa Rasilimali Watu katika Taasisi za Umma.

Lengo la Ukaguzi huo ni:-

(i) Kupima na kuangalia ni kwa kiwango gani, Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika kusimamia masuala ya Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

(ii) Kuona kama matokeo ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu yanafikiwa kama ilivyotarajiwa.

### 2.1.1 Maeneo yanayokaguliwa

Maeneo yanayokaguliwa katika Ukaguzi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma ni pamoja na:-

a) Ajira
b) Upandishaji vyeo
c) Upimaji wa wazi wa Utendaji Kazi (OPRA)
d) Mafunzo
e) Likizo ya mwaka
f) Likizo ya ugonjwa
g) Nidhamu

Katika maeneo hayo, Ukaguzi hufanyika kwa kutumia Mfumo wa ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria wa masuala ya Rasilimali watu wa Tume ambao msingi wake umeundwa kutokana na:-

(i) Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma (2008)
(ii) Sheria ya msingi ambayo ni Sheria ya Utumishi wa Umma, Na.8 ya Mwaka 2002 na Marekebisho yake.
(iii) Sheria zinazofuatia ambazo ni:-

- Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka (2003)
- Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma (2009)
- Nyaraka
- Taratibu za Uendeshaji
- Taratibu bora za uendeshaji katika masuala ya Ajira na Nidhamu
- Miundo ya Utumishi.

### 2.1.2 Aina ya Ukaguzi

Tume hufanya Ukaguzi wa aina mbili;

(i) Ukaguzi wa kawaida.

Ukaguzi huu hufanyika kila mwaka baada ya mwaka wa fedha husika kuisha.

(ii) Ukaguzi maalum.

Ukaguzi huu hufanyika kufuatia maagizo ya Mkuu wa Utumishi wa Umma, mambo yaliyobainishwa kwenye ukaguzi wa kawaida, malalamiko yaliyowasilishwa na watumishi wa Umma Tume na taarifa za utekelezaji wa masuala ya Rasilimali Watu zinazowasilishwa Tume na Waajiri mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Lengo la ukaguzi huu ni kubaini ukweli wa malalamiko yaliyowasilishwa pamoja na kurekebisha upungufu uliopo kabla athari zaidi hazijatokea kwa maeneo ambayo kulikuwa na ukiukwaji wa utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

### 2.1.3 Ukaguzi uliofanyika

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17, Tume imefanya ukaguzi katika Taasisi **41.** Taasisi hizo ni Sekretarieti za Mikoa mitano (**5**) ambayo ni Morogoro, Iringa, Mbeya, Arusha na Mwanza, Mamlaka za Serikali za Mitaa **30** zilizopo katika mikoa hiyo pamoja na Wakala na Taasisi sita **(6)**. Taasisi zilizokaguliwa zimepelekewa Hoja za ukaguzi ambazo zinapaswa kujibu.

Kupitia kaguzi hizi Tume imebaini kuwa baadhi ya Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu hazitekelezi ipasavyo majukumu yao hususan katika usimamizi wa masuala ya Ajira na Nidhamu na kuwepo kwa muitikio usioridhisha wa utekelezaji wa Mfumo wa Upimaji Utendaji kazi wa Wazi (OPRAS).

## 2.2 Kushughulikia Rufaa na Malalamiko

Majukumu mengine ya msingi ya Tume ni kushughulikia Rufaa na Malalamiko yanayowasilishwa Tume na Watumishi wa Umma ambao hawajaridhika na uamuzi wa Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu.

### 2.2.1 Uamuzi wa Tume kuhusu rufaa

Tume katika uamuzi wa rufaa hutoa uamuzi wa aina tatu.

(i) Kukataa rufaa, ni pale ambapo tuhuma zimethibitika na Mamlaka za Nidhamu zimezingatia hatua za kuwachukulia hatua za nidhamu watumishi walio chini yao

(ii) Kuikubali rufaa, ni pale ambapo tuhuma hazikuthibitika ama Mamlaka za Nidhamu zimekiuka Sheria, Kanuni na Taratibu katika kuwachukulia hatua za kinidhamu. Aidha, baadhi ya rufaa Tume huzikubali na kuagiza mashtaka yaanze upya.

(iii) Kubatilisha adhabu, Tume ina uwezo wa kubatilisha adhabu iliyotolewa na Mamlaka ya Nidhamu kulingana na uzito wa makosa yaliyotendwa na mrufani.

Hivi karibuni Tume ilifanya mkutano wake wa tatu katika mwaka huu wa fedha **2016/17**. Katika mkutano huu Rufaa **48** na Malalamiko matatu **(3)** yaliwasilishwa mbele ya Tume kwa uamuzi. Kati ya hizo, Rufaa **32** zimekataliwa. Rufaa **13** zimekubaliwa kati ya hizo, Rufaa mbili **(2)** Tume imeagiza mashtaka yaanze upya baada ya kubaini kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Rufaa moja **(1)** ilikataliwa kwa sababu ilikatwa nje ya muda uliotolewa kisheria. Aidha, Rufaa moja **(1)** imeahirishwa kutolewa uamuzi na Rufaa moja **(1)** inasubiri uamuzi wa Mahakama.

Kwa upande wa malalamiko Tume imetoa uamuzi wa Malalamiko 3 yaliyopokelewa ambapo malalamiko mawili **(2)** yamekubaliwa na lalamiko moja **(1)** limerejeshwa kwenye Mamlaka husika ili liweze kushughulikiwa.

## 2.3 Kuwezesha Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu

Tume ina jukumu la kuwezesha na kuelimisha Wadau wake juu ya utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni na Taratibu zilizopo za kusimamia Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma. Uwezeshaji huo hufanyika kwa kupitia:-

a) Kutoa Miongozo na Maelekezo yanayowezesha Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu kuwa na tafsiri moja ya utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

b) Ziara za Makamishna kwenye Taasisi mbalimbali za Umma zinazowakutanisha na Watendaji pamoja na watumishi

kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu Tume na usimamizi wa masuala ya Rasilimali watu.

c) Vikao vya kazi vinavyoandaliwa na Tume au vinavyofanywa na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu.

d) Vyombo vya habari (vipindi vya redio na televisheni pamoja na makala katika magazeti).

## 2.4 Kufuatilia Utekelezaji wa Usimamizi wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma kwa Waajiri

Tume ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa usimamizi wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma kwa lengo la:-

(i) Kufahamu hali ya usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

(ii) Kufahamu jinsi Mamlaka zinavyotekeleza masuala ya usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

(iii) Changamoto zilizopo katika usimamizi wa Rasilimali watu

(iv) Kuiwezesha Tume kutoa taarifa kwa Serikali juu ya hali ya usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

Jukumu hili hutekelezwa kupitia Taarifa zinazowasilshwa kwa mujibu wa Mwongozo wa kuwasilisha taarifa Tume.

Kupitia Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kipindi cha Robo ya Pili (Oktoba- Desemba 2016) Tume ilibaini kuwa bado Taasisi nyingi za Umma hazitekelezi wajibu wao wa kuwasilisha Taarifa husika kwa wakati. Hivyo, Tume inaziagiza Mamlaka za Ajira na Nidhamu kuwasilisha Taarifa zinazohusu Utekelezaji wa Usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Mwongozo wa uwasilishaji wa taarifa hizo.

## 3.0 CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA KATIKA USIMAMIZI WA UENDESHAJI WA RASILIMALI WATU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Tume kupitia Ukaguzi wa masuala ya Rasilimali Watu na kushughulikia Rufaa imebaini changamoto mbalimbali katika usimamizi wa Rasilimali Watu ambazo ni pamoja na:-

(i) Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu kushindwa kuwachukulia hatua kwa wakati au kutokuchukua hatua kabisa dhidi ya watumishi wanaofanya makosa au wenye utendaji usioridhisha walio chini yao.

(ii) Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu, kutokuunda Kamati za Uchunguzi au kutumia Taarifa za Uchunguzi wa awali kama zilivyowasilishwa kwao.

(iii) Upungufu katika uandaaji wa mashtaka na uendeshaji wa mchakato mzima wa mashauri ya kinidhamu.

(iv) Upungufu katika uandishi wa Taarifa za Kamati za Uchunguzi na taarifa ya mwenendo wa uchunguzi mathalan baadhi kutokuwa na hadidu za rejea.

(v) Baadhi ya Waajiri na Mamlaka za Nidhamu kutoa uamuzi nje ya muda, kuchelewa kumtaarifu mtuhumiwa uamuzi uliofikiwa na kufanya uzembe wakati wa kuandika barua za uamuzi.

(vi) Baadhi ya Waajiri na Mamlaka za Nidhamu kukaa muda mrefu na mashauri ya nidhamu pasipo kuyahitimisha.

(vii) Baadhi ya Waajiri kutoa barua inayoonyesha anatoa adhabu wakati yeye si Mamlaka ya Nidhamu.

(viii) Baadhi ya Waajiri kutoelewa tofauti kati ya kutoa maelekezo na utoaji adhabu kwa watumishi wanaoenda kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu.

(ix) Watumishi kutokutambua haki zao, kama vile kuhoji mashahidi, haki ya kujitetea na kujua mahali sahihi pa kukata rufaa dhidi ya maamuzi yanayotolewa.

(x) Baadhi ya watumishi wa Umma kutozingatia maadili ya Utumishi na maadili ya kazi zao.

### 3.1 Hatua ambazo Tume imechukua

Hatua ambazo Tume imekuwa ikizichukua kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Kutoa maelekezo ya namna ya kuboresha maeneo yenye upungufu kwa Taasisi zilizokaguliwa.

(ii) Kuziandikia Taasisi za Umma zinazopatikana na hoja za ukaguzi ili ziweze kujibu

(iii) Kuwaarifu Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu (UTUMISHI) na Mamlaka zinazosimamia Taasisi husika kuchukua hatua stahiki kwa Taasisi hizo.

(iv) Kuendelea kuwaelimisha Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu kupitia ziara za Makamishna, vyombo vya habari na kutoa maelekezo kwa njia ya Miongozo.

## 4.0 MAMBO YA KUZINGATIA

Ili kuhakikisha kuwa kuna kuwepo na utawala bora katika usimamizi na uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma Tume inasisitiza Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu na watumishi wa Umma kuzingatia mambo yafuatayo;-

a) Taasisi zinazokaguliwa na kupatikana na Hoja za Ukaguzi kujibu ipasavyo hoja hizo na kujirekebisha.

b) Watendaji Wakuu wa Taasisi wasimamie ipasavyo watumishi walio chini yao na kuwachukulia hatua stahiki wanapokiuka Maadili ya Kazi zao.

c) Watumsihi wa Umma na Watendaji wafahamu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazowaongoza katika utendaji wao na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

d) Watumishi wa umma wazingatie Maadili ya Utumishi wa Umma na ya Taaluma zao.

e) Kupunguza gharama kubwa kwa Serikali kwa watumishi wanaokata Rufaa na kushinda kesi kutokana na Waajiri/Mamlaka za Ajira na Nidhamu kutojua Sheria stahiki za kuwachukulia hatua watumishi wanaokwenda kinyume na maadili.

f) Mamlaka za Ajira na Nidhamu zihakikishe zinatoa uamuzi sahihi na kwa wakati na kuepuka kupindisha taratibu za mashauri ya nidhamu, kuajiri watumishi wasio na sifa na wasiowajibika.

g) Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu ziwasilishe taarifa za utekelezaji wa masuala ya kiutumishi Tume kwa mujibu wa Mwongozo wa kuwasilisha taarifa Tume.

## 5.0 HITIMISHO

Tume ya Utumishi wa Umma inatoa wito kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu ili kuimarisha Utawala Bora katika Utumishi wa Umma. Aidha, kwa upande wa Watumishi wa Umma,Tume inawasisitiza watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia Maadili ya Utumishi wa Umma na ya Taaluma zao.